SHERIA ZA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA) KAMA ZILIVYOFANYIWA MAREKEBISHO MWAKA 2002
(SURA YA 287)
HALMASHAURI YA KIJIJI CHA ……

SHERIA NDOGO.
(Zimetungwa chini ya kifungu cha 163
SHERIA NDOGO ZA (KUDHIBITI UUZAJI NA UNYWAJI WA POMBE SAA ZA KAZI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO ZA MWAKA 2014.

Jina na mwanzo wa kuanza kutumika	**1**.Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Kudhibiti Uuzaji na Unywaji wa Pombe Saa za Kazi) za Halmashauri ya Kijiji cha …… za mwaka 2014 na zitaanza kutumika baada ya kuidhinishwa na Halmashauri.ya Wilaya ya Rombo.
Maeneo ya matumizi	**2.**Sheria Ndogo hizi zitatumika katika maeneo yote ya Kijiji cha ……. … Halmashauri ya Wilaya ya Rombo.
Tafsiri	**3.** Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo:- "Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Rombo. "Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi. "Afisa Muidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeidhinishwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi. "Mmiliki au Mfanyabiashara" maana yake ni pamoja na mtu,taasisi binafsi, kampuni, taasisi ya umma,kikundi cha watu anayemiliki/inayomiliki/kinachomiliki baa ya pombe zisizo za kienyeji,baa ya pombe za kienyeji,grosari,mgahawa,hoteli na klabu ambapo pombe ya aina yeyote isiyo ya kienyeji itauzwa ndani yake. "Wakala" maana yake ni Serikali ya Kijiji ambayo kwa niaba ya Halmashauri itahakikisha sehemu zote zinazouza pombe ya aina yeyote ile zinafunguliwa kwa wakati,uuzaji, ununuaji na unywaji wa pombe unafanyika kwa wakati kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi. "Baa, grosari,mgahawa,hoteli,klabu"maana yake ni sehemu yeyote au mahali popote ambapo pombe huuzwa rejareja. "Pombe"maana yake ni vinywaji visivyo vya kienyeji vinavyolewesha na vinywaji vya kienyeji vinavyolewesha.

	“Pombe ya kienyeji” maana yake ni pombe ya mbege,asali iliyochachushwa(kangara),ulanzi,tembo,dengerua,dadii pamoja na pombe nyinginezo zilizo katika kundi hili chini ya Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. “Pombe isiyo ya kienyeji”maana yake ni bia,mvinyo,spiriti pamoja na pombe nyinginezo zilizo katika kundi hili chini ya Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania “Saa za kazi”maana yake ni muda wowote ule uliokatazwa kuuza,kununua na kunywa pombe ya aina yeyote chini ya Sheria Ndogo hizi. “Moshi”maana yake ni pombe haramu ya gongo. “Kibali au Leseni”maana yake ni idhini ya maandishi itolewayo chini ya Sheria za Jamhuri ya muungano wa Tanzania na chini ya Sheria Ndogo hizi kwa lengo la kuendesha shughuli yeyote iliyo halali. “Maeneo ya kijijini”maana yake ni sehemu nyingine isiyojumuisha maeneo ya mijini kama jiji,Manispaa na Halmashauri ya Mji ndani ya Jamhuri ya muungano wa Tanzania,maeneo haya yako chini ya Halmashauri za Wilaya. “Mji mdogo”kwa maana ya Sheria Ndogo hizi, ni maeneo yanayochipukia na kukua kama Mji lakini bado yako ndani ya Vijiji, maeneo haya yako chini ya Halmashauri za Wilaya. “Tozo ya adhabu”maana yake ni faini anayolipa mtu yeyote,mmiliki au mfanyabiashara, kikundi cha watu,taasisi binafsi au taasisi ya umma aliyekwenda/kilichokwenda/iliyokwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi. “Mtu” maana yake ni mtu asilia au mtu kisheria kama vile kampuni, shirika,au kikundi cha watu au jumuiya. “Mnywaji wa pombe”maana yake ni mtu yeyote anayetumia kinywaji chenye kilevi. “Dola”maana yake ni Jeshi la Polisi au Mgambo. “Mahakama”Maana yake ni Chombo cha mwisho Kisheria chenye uwezo au mamlaka ya kuendesha mashauri na kutoa maamuzi.

	"Sheria Kuu"Maana yake ni Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania(Sheria ndogo za Halmashauri haziusishwi hapa).
Muda wa kufungua na kufunga sehemu za kuuzia pombe zisizo za kienyeji,maeneo ya Miji Midogo na Kijijini/ Muda wa kuuza, kununua na kunywa pombe zisizo za kienyeji,maeneo ya Miji Midogo na Kijijini	**4.**(1)Sehemu yeyote au mahali popote pasipohusisha Hotel au Mgahawa ambapo pombe zisizo za kienyeji zitauzwa rejareja ni sharti pafunguliwe saa 9:30 Alasiri na kufungwa saa 2:00 usiku, kwa siku za Jumatatu mpaka Ijumaa. (2)Sehemu yeyote au mahali popote pasipohusisha Hotel au Mgahawa ambapo pombe zisizo za kienyeji zitauzwa rejareja ni sharti pafunguliwe saa 8:00 mchana na kufungwa saa 4:00 usiku, kwa siku za Jumamosi mpaka Jumapili na siku za Sikukuu. (3)Sehemu yeyote au mahali popote panapohusisha Hoteli ambapo pombe zisizo za kienyeji zitauzwa rejareja ni sharti pafunguliwe saa 9:30 Alasiri na kufungwa saa 2:00 usiku, kwa siku za Jumatatu mpaka Ijumaa. (4)Sehemu yeyote au mahali popote panapohusisha Hotel ambapo pombe zisizo za kienyeji zitauzwa rejareja ni sharti pafunguliwe saa 8:00 mchana na kufungwa saa 4:00 usiku, kwa siku za Jumamosi mpaka Jumapili na siku za Sikukuu. (5)Sehemu yeyote au mahali popote panapohusisha Mgahawa ambapo pombe zisizo za kienyeji zitauzwa rejareja ni sharti pafunguliwe kati ya saa 9:00 Alasiri mpaka saa12:00 jioni. (6)Kifungu cha 4(5) kitajumuisha siku zote za wiki pamoja na siku za sikukuu ambapo mteja atakuwa ndani ya Mgahawa. (7) Sehemu yeyote au mahali popote panapohusisha nyumba ya kulala wageni chini ya Leseni ya Hoteli ambapo pombe zisizo za kienyeji zitauzwa rejareja,ni sharti mgeni huyo aandikishe jina lake kwenye kitabu cha wageni,akabidhiwe chumba chake ndipo aweze kuuziwa pombe, anaweza kuuziwa pombe wakati wowote kwa siku nzima au usiku mzima akiwa maeneo ya ndani ya Hoteli. (8)Mkurugenzi Mtendaji anayo mamlaka ya kutoa leseni ya muda ya kuuza pombe zisizo za kienyeji mahali popote penye mkusanyiko maalum,hafla au dhifa maalum,sikukuu au sherehe maalum. (9)Isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo,leseni iliyotolewa chini ya kifungu cha 4(8) itaruhusu pombe zisizo za kienyeji kuuzwa na kununuliwa saa 8:00 mchana mpaka saa 4:00 usiku siku za Jumamosi na Jumapili.

	(10)Muda wa matumizi ya leseni iliyotolewa chini ya kifungucha4(8-9) unaweza kuongezwa mfululizo kwa kutuma maombi maalum kwa Afisa Muidhiniwa,lakini pale maombi yatakapokubalika muda huo hautazidi siku tatu.
Muda wa kufungua na kufunga sehemu za kuuzia pombe za kienyeji,maeneo ya Miji Midogo na Kijijini/ Muda wa kuuza, kununua na kunywa pombe za kienyeji,maeneo ya Miji Midogo na Kijijini	**5.**(1)Sehemu yoyote au mahali popote ambapo pombe za kienyeji zitauzwa rejareja ni sharti pafunguliwe saa 10:00 Jioni na kufungwa saa 2:00 Usiku, kwa siku za Jumatatu mpaka Ijumaa. (2) Sehemu yeyote au mahali popote ambapo pombe za kienyeji zitauzwa rejareja ni sharti pafunguliwe saa 9:00 Alasiri na kufungwa saa 4:00 usiku, kwa siku za Jumamosi na Jumapili na siku za Sikukuu. (3)Isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo,masharti ya kifungu cha 4(8-10) yatatumika mahali pengine pale ambapo leseni ya muda ya kuuza na kununua pombe za kienyeji imeombwa kutolewa na maombi yakakubalika.
Mamlaka ya Afisa Muidhiniwa	**6.**(1)Afisa Muidhiniwa anayo mamlaka ,miongoni mwa mambo yote,kuingia wakati wowote unaofaa katika ardhi,jengo,nyumba au sehemu yoyote ndani ya eneo la himaya yake ili kufanya ukaguzi,kuhoji au kufanya kazi yeyote chini ya masharti ya Sheria Ndogo hizi. (2) Katika kutekeleza majukumu yake Afisa Muidhiniwa anaweza kutumia Jeshi la Polisi au Mgambo. (3)Afisa Muidhiniwa anayo mamlaka kwa kufuata taratibu, kukamata na kushikilia pombe au vitendea kazi vya mmiliki endapo mmiliki ataenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi. Endapo mmiliki atatii masharti ya Sheria Ndogo hizi za pombe, atatoa tozo la Shilingi elfu ishirini (20,000/=) kama adhabu na pombe na vyombo vyake vilivyokamatwa vitarejeshwa, lakini mfanyabiashara huyo atakuwa chini ya maangalizo kwa kipindi cha miezi mitatu mfululizo. Endapo mmiliki atashindwa kuchukua pombe au vitendea kazi vyake vilivyokamatwa kwa muda uliopangwa,Halmashauri itatoza shilingi elfu moja (Tsh.1,000/=) kama gharama ya ulinzi kwa kila siku itakayozidi mpaka tarehe ambayo tozo ya adhabu (faini) italipwa. (4)Afisa Muidhiniwa anayo mamlaka ya kuuza kwa kufuata taratibu, pombe au vitendea kazi vya mmiliki vilivyokamatwa endapo mmiliki atashindwa kulipa fedha anazodaiwa kama tozo ya adhabu kwa muda uliopangwa.

	(5)Afisa Muidhiniwa anayo mamlaka kwa kufuata taratibu, kumkamata na kumfungulia mashtaka mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi. (6)Afisa Muidhiniwa anayo mamlaka kwa kufuata taratibu, kumfungia leseni ya biashara mmiliki au mfanyabiashara atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi. (7)Afisa Muidhiniwa anayo mamlaka kwa kufuata taratibu, kumfutia leseni ya biashara mmiliki au mfanyabiashara atakayeonekana kuwa sugu kwa kukiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi. (8)Afisa Muidhiniwa anayo mamlaka kwa kufuata taratibu,kumtaka mtu yeyote,mmiliki au mfanyabiashara atakayekutwa na kosa na kukiri kosa hilo chini ya Sheria Ndogo hizi, kulipa tozo ya adhabu au kushiriki katika kufanya kazi kwenye miradi ya umma au kazi zozote zenye maslahi kwa jamii kwa muda ambao utakuwa unalingana na kiasi cha tozo ya adhabu anayotakiwa kulipa.
Uhusiano na Sheria kuu	**7.**(1)Sheria Ndogo hizi hazizuii au vinginevyo hazimuondolei mtu yeyote kosa la jinai chini ya Sheria za nchi, mtu yeyote atakayepatikana na hatia ya makosa mengine iwe yametendeka wakati afisa muidhiniwa anatekeleza wajibu wake,ama yametendeka wakati afisa muidhiniwa hayupo katika kutekeleza wajibu wake. (2)Mtu yeyote hataadhibiwa chini ya Sheria Ndogo hizi endapo ameshafunguliwa mashtaka na kusikilizwa chini ya Sheria kuu. (3)Uendeshaji wa mashtaka ya makosa chini ya Sheria Ndogo hizi utasimamishwa mara mashtaka ya jinai chini ya Sheria kuu yatakapofunguliwa. (4)Sheria Ndogo hizi hazihusishi utumiaji wa pombe haramu ya moshi. (5)Kwa vyovyote vile itakavyoonekana inafaa mamlaka ya utoaji leseni inaweza kupunguza muda au kurefusha muda wa kuuza,kununua au kunywa pombe pale ambapo taratibu za Sheria Kuu zimefuatwa.

Makosa	**8.**(1) Itakuwa ni makosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi iwapo:- (i) Mmiliki au Mfanyabiashara atafungua baa,grosari,mgahawa,hoteli au klabu na kuuza pombe saa za kazi chini ya Sheria Ndogo hizi. (ii) Mtu yeyote atanunua na kunywa pombe saa za kazi chini ya Sheria Ndogo hizi. (iii) Mtu yeyote atakunywa pombe saa za kazi chini ya Sheria Ndogo hizi. (iv) Mtu yeyote ataingilia na kuhujumu kazi za afisa muidhiniwa wakati anatekeleza majukumu yake. (v) Mtu yeyote atadharau amri halali ya afisa muidhiniwa chini ya Sheria Ndogo hizi. (vi) Mtu yeyote atakataa au atashawishi watu wengine au atamshawishi mtu mwingine kukataa kutekeleza masharti ya Sheria Ndogo hizi. (vii) Mtu yeyote atasababisha au kufanya fujo au atatumia lugha ya matusi katika eneo la mmiliki au mfanyabiashara.
Adhabu	**9.**(1)Mmiliki au mfanyabiashara atakayeshindwa kutekeleza masharti ya Sheria Ndogo hizi au atakayevunja Sheria Ndogo hizi na kutiwa hatiani chini ya kifungu cha 4(1-10) atatozwa tozo ya adhabu (faini) isiyozidi Shilingi za Kitanzania (100,000/=) laki moja au kifungo kizichozidi miezi 12 au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo au kushiriki katika kufanya kazi kwenye miradi ya umma au kazi zozote zenye maslai kwa jamii kwa muda ambao utakuwa unalingana na kiasi cha faini anayotakiwa kulipa. (2)Mnywaji wa pombe atakayeshindwa kutekeleza masharti ya Sheria Ndogo hizi au atakayevunja Sheria Ndogo hizi na kutiwa hatiani chini ya kifungu cha 4(1-10) atatozwa tozo ya adhabu (faini) isiyozidi Shilingi za Kitanzania (50,000/=) elfu hamsini au kifungo kizichozidi miezi 6 au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo au kushiriki katika kufanya kazi kwenye miradi ya umma au kazi zozote zenye maslai kwa jamii kwa muda ambao utakuwa unalingana na kiasi cha faini anayotakiwa kulipa. (3) Mmiliki au mfanyabiashara atakayeshindwa kutekeleza masharti ya Sheria Ndogo hizi au atakayevunja Sheria Ndogo hizi na kutiwa hatiani chini ya kifungu cha 5(1-3) atatozwa tozo ya adhabu (faini) isiyozidi Shilingi za Kitanzania (100,000/=) laki moja au kifungo kizichozidi miezi 12 au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo au kushiriki katika kufanya kazi kwenye miradi ya umma au kazi zozote zenye maslai kwa jamii kwa muda ambao utakuwa unalingana na kiasi cha faini anayotakiwa kulipa.

	(4)Mnywaji wa pombe atakayeshindwa kutekeleza masharti ya Sheria Ndogo hizi au atakayevunja Sheria Ndogo hizi na kutiwa hatiani chini ya kifungu cha 5(1-3) atatozwa tozo ya adhabu (faini) isiyozidi Shilingi za Kitanzania (50,000/=) elfu hamsini au kifungo kizichozidi miezi 6 au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo au kushiriki katika kufanya kazi kwenye miradi ya umma au kazi zozote zenye maslai kwa jamii kwa muda ambao utakuwa unalingana na kiasi cha faini anayotakiwa kulipa. (5) Mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya Sheria Ndogo hizi au atakayevunja Sheria Ndogo hizi na kutiwa hatiani chini ya vifungu vingine isipokuwa kifungu cha 4(1-10) na 5(1-3) atatozwa tozo ya adhabu (faini) isiyozidi Shilingi za Kitanzania (50,000/=) elfu hamsini au kifungo kizichozidi miezi 12 au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo au kushiriki katika kufanya kazi kwenye miradi ya umma au kazi zozote zenye maslai kwa jamii kwa muda ambao utakuwa unalingana na kiasi cha faini anayotakiwa kulipa. (6)Mkurugenzi Mtendaji anao uwezo wa kumtoza mtu yeyote tozo ya adhabu(faini), isiyozodi Shilingi za Kitanzania (20,000/=) elfu kumi, endapo mkosaji atakiri kwa maandishi kutenda kosa hilo na kukubali kulipa kiasi anachodaiwa chini ya Sheria Ndogo hizi. (Compounding Offence).

HATI YA KUKIRI KUTENDA KOSA

Mimi …….nakiri mbele ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo,kwamba mnamo tarehe……
Mwezi……..nilitenda kosa kwa kukiuka kifungu cha ……cha Sheria Ndogo za (Kudhibiti Uuzaji na Unywaji wa Pombe Saa za Kazi) za Halmashauri ya Wilaya ya Rombo za mwaka 2014.

Nipo tayari kulipa kiasi ninachodaiwa kama tozo ya adhabu, ikiwa Mkurugenzi Mtendaji ataamua kutekeleza madaraka yake aliyopewa chini ya kifungu cha 9(6) cha Sheria Ndogo hizi.

Nathibitisha kwamba yote niliyosema hapo juu ni kweli kwa kadri ya ufahamu wangu.

Jina…….

sahihi…….

Tarehe……

Wadhifa……..

Muhuri wa Kijiji ulibandikwa kwenye Sheria ndogo hizi kwa kufuata azimio lililopitishwa kwenye mkutano mkuu wa kijiji uliofanyika tarehe …….. mbele ya:

…….
MWENYEKITI WA KIJIJI

……...
MTENDAJI WA KIJIJI

UMEWEKWA

……..
MUHURI WA HALMASHAURI YA KIJIJI

ZIMETHIBITISHWA NA KUKUBALIWA NA BARAZA LA MADIWANI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO KATIKA MKUTANO WA BARAZA TAREHE …… MWEZI …….. MWAKA ……. MBELE YA:

…….
ANTHONY .J. TESHA
MWENYEKITI WA HALMASHAURI (W)
ROMBO

……..

JUDETHADEIUS .J. MBOYA
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
ROMBO

IMEBANDIKWA

……..

LAKIRI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO

-*